JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHIRIKA LA ELIMU KIBAHA
S.L.P 30054, Kibaha. Simu: 023 2402142, Fax: 0232402324,
Barua Pepe:kec@kec.or.tz/Tovuti:www.kec.or.tz

Shule ya Sekondari Kibaha

Kumb.Na.KSS/…….
Tarehe:……..

Ndugu:……
……..

YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUINGIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha KWANZA mwaka wa masomo wa 2024. Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe 08/01/2024.

Shule iko kilometa 40 kutoka Dar es Salaam karibu na Kiwanda cha TANCHIN zamani TAMCO Scania kilicho upande wa kulia mwa barabara inayoelekea Morogoro). Fuata barabara iliyo kushoto ukitokea Dar es Salaam hadi Tumbi Hospitali kilipo kituo cha mabasi nje ya Geti dogo la Hospitali. Uliza njia ya kuelekea shule ya Sekondari Kibaha.

Yafuatayo ni maelezo na maagizo ambayo unashauriwa kuyatimiza kabla hujafika hapa shuleni.

1. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**
   - (i) Fika shuleni ukiwa na cheti cha kuzaliwa.
   - (ii) Fika na Fomu ya kupimwa afya ikiwa imejazwa na Daktari wa serikali
   - (iii) Fika na jalada la kutunzia mitihani
   - (iv) Fika shuleni ukiwa na kadi ya BIMA ya afya

2. **SARE YA SHULE:**
   - (i) Unatakiwa uwe na suruali mbili (DARK-BLUE) ya malinda,pindo na mifuko.
   - (ii) Mashati mawili (MEUPE) ya mikono mifupi yenye **Nembo ya Shule**.
   - (iii) Tai rangi ya bluu yenye michirizi mweupe.
   - (iv) Fulana (T-shirt) nyeupe yenye kola na **Nembo ya Shule**.
   - (v) Nguo rasmi za kushindia ambazo ni;
     - Suruali mbili za rangi ya maroon au damu ya mzee zisizo na malinda.
     - Tshirt mbili rangi ya zambarau zenye **Nembo ya Shule**.

TANBIHI:

(i) Ili kutoleta utofauti wa sare, unashauriwa kushona sare hizo kwa fundi anayepatikana karibu na maeneo ya shule kwa maelezo zaidi piga namba 0652 136963.

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani,hivyo siku ya kuripoti aje akiwa amevaa TRACK SUIT ya rangi ya bluu (Chelsea).

(vi) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga na Kamba, jozi moja au zaidi visivyochongoka wala kuinuka mbele.

(vii) Soksi fupi jozi mbili au zaidi za rangi nyeusi na zisizo na mapambo yoyote.

(viii) Aje na mkanda mweusi wa ngozi wa suruali wenye "buckle" ndogo.

(ix) Bukta au kaptura na jezi yake rangi ya bluu (Chelsea) kwa ajili ya michezo na kazi za mikono.

(x) Raba nyeupe za michezo jozi moja (01).

(xi) Aje na sweta la rangi ya "dark-blue" yenye shingo ya herufi 'V'.

3. MAHITAJI MENGINE:

(i) Kila mwanafunzi awe na Sahani, Bakuli, Kikombe, Kijiko kwa ajili ya chakula.

(ii) Aje na Shuka mbili za bluu bahari, mto na Foronya mbili, pamoja na Chandarua. (ukipenda unaweza kuleta blanketi moja ingawa hali ya hewa ya Kibaha ni ya joto. Vile vile ulete taulo moja ya kuogea na vifaa vingine vya usafi wa binafsi.

(iii) Aje na ndoo 2 za lita 10 kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa na kuoga.

(iv) Aje na Ndala kwa ajili ya kuogea.

(v) Toilet Paper kumi (10) au zaidi.

(vi) Godoro moja lenye ukubwa wa (200 x 80)cm

(vii) Trunker la bati la kufunga kwa kufuri.

(viii) Aje na nguo za michezo (track suit na bukta moja rangi ya bluu.

(ix) Mpatie mwanao hela ya matumizi binafsi ikiwemo dharula na matibabu.

(x) Karatasi za kudurufia (photocopying papers), ream moja (1)

(xi) Mfagio laini (soft broom) mmoja (1)

(xii) Jembe moja(1) na mpini wake.

NB: Ili kupunguza usumbufu wa kuja na godoro,unaweza ukalipata karibu na shule Kwa mawasiliano piga namba 0717 002439.

4. VIFAA MAALUMU:

(i) Anatakiwa aje na Mathematical set (Mkebe wa vifaa vya Mahesabu) moja.

(ii) Kwa upande wa masomo, anatakiwa kuleta daftari kubwa (4 -QUIRE) zisizopungua 15 za kutosha kuandikia katika masomo yako yote.

(iii) Anatakiwa awe na nauli ya kurudia nyumbani wakati wa likizo. ambapo shule ina utaratibu wa kuwatafutia mabasi

(iv) Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki **Simu, line, chaja, redio, pasi, laptop, MP3, au kifaa chochote cha mawasiliano** shuleni. Akipatikana na vitu hivyo **atakufukuzwa** shule na vifaa vitaharibiwa.

TANBIHI:

A. Endapo mwanafunzi/mzazi/mlezi atakuwa na dharura awasiliane kwa kutumia namba zifuatazo :-

(i) 0717 002439 Makamu Mkuu wa Shule
(ii) 0754 292351 Mtaaluma
(iii) 0717 694581 Mwl, nidhamu
(iv) 0652 136963 Mwl, malezi

B. Wakati wa likizo ya kurudi nyumbani mwanafunzi lazima asafiri chini ya utaratibu wa shule uliopo.

5. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI.

(i) Kumiliki **Simu,line,chaja,redio,pasi, laptop,MP3, au kifaa chochote cha mawasiliano** shuleni.
(ii) Wizi, uasherati, ubakaji na ushoga.
(iii) Ulevi, uvutaji bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
(iv) Makosa ya jinai.
(v) Kupigana au kupiga
(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(vii) Kudharau Bendera ya Taifa.
(viii) Kuoa
(ix) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama.
(x) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(xi) Kufumbia makosa/uovu shuleni.

6. Mwisho natumia fursa hii kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shuleni na naamini utatumia vizuri nafasi hii uliyopewa na Taifa ya kukuongezea elimu yako.

Karibu sana.

……..
GEORGE M. KAZI
Mkuu wa Shule,
SHULE YA SEKONDARI KIBAHA.
SIMU YA MKONONI: 0766 591719

Nakala kwa: Maafisa Elimu (M)
MIKOA YOTE YA TANZANIA BARA – Taarifa kwa wanafunzi

Anuani……

…….
. Tarehe: ……..

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Kibaha,
S.L.P. 30053,
KIBAHA

YAH: <u>BARUA YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII</u>

Asante kwa barua yako Kumb.Na……ya tarehe ……..

(a) Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha Kwanza kwa mwaka……
(b) Niko tayari/siko tayari kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya Kibaha Sekondari
(c) Nitahudhuria/Sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hapa shuleni
(d) Nikishindwa kuhudhuria bila sababu ya msingi nifukuzwe shule.
(e) Nitaleta/Sitaleta
    (i) Uthibitisho wa Uraia/Cheti cha kuzaliwa
    (ii) Vitu vinavyohitajika kwa matumizi yangu
    (iii) Cheti cha Afya
    (iv) Fomu ya kuandikishwa na habari zangu za mzazi/mlezi wangu.

Asante.

……. ……
JINA LA MWANAFUNZI **SAINI YA MWANAFUNZI**

FOMU YA KUANDIKISHA SHULENI NA HABARI ZA WAZAZI WA MWANAFUNZI
SEHEMU A: (HABARI ZA MWANAFUNZI):

1. Jina kamili (Kama kwenye mtihani)……...
2. Tarehe ya kuzaliwa ……Dini ……Dhehebu ……
3. Mahali na Wilaya ulipozaliwa …….
4. Shule ulipomaliza darasa la saba……
   Mwaka uliomaliza ……
5. Kidato unachokuja kuingia hapa shule ya Sekondari ya Kibaha ……
6. Namba yako ya mtihani darasa la saba ilikuwa ……..
7. Michezo unayopendelea:

	JINA LA MCHEZO	**MAHALI/SHULE**	**MWAKA**
1			
2			
3			
4			
5			

8. Kazi yeyote ya uongozi uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k.

MADARAKA AU UONGOZI	**SHULE/MAHALI**	**MWAKA**

9. Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo (kama vile michezo, mpira, bustani, ushonaji viatu, nguo, michezo ya kuigiza). kuimba
   1……2…… 3. ……..
10. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi (wa kiume/wa kike) k.m. Mjomba, mama, shangazi, kaka, dada kufuatana na umri wao wa kuzaliwa.

	JINA LA NDUGU	**KAZI ANAYOFANYA**	**UHUSIANO NA MWANAFUNZI**	**KIWANGO CHA ELIMU**	**ANUANI**	**NAMBA YA SIMU**
1.						
2.						
3.						
4.						
5.						

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kweli. Naahidi kuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe:……..Saini ya Mwanafunzi ……

SEHEMU B: (HABARI ZA MZAZI/MLEZI):

1. Jina kamili……

2. Kazi yake. ……

3. Mahali anapoishi …….....
   Anwani ya nyumbani ……
   Kijiji …….Kata ……
   Tarafa ……Wilaya …….Mkoa……..

4. (a) Anuani ya Mahali pa kazi ya mzazi/mlezi ……
   (b) Nambari ya simu ……..

5. Dini ya mzazi …….. Madhehebu ……

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo.
   ……

7. Anwani ya kazini (ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu na kila mara inapobadilika tunaomba utuarifu rasmi kwa barua kupitia Mkuu wa Kata, Tarafa au wa Kijiji chako)…….
   ……

8. Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni za kweli.

9. Naahidi kushirikiana na walimu kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe ……Saini ya Mzazi/Mlezi ……

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
KIBAHA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 30053,
KIBAHA

SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

The Medical Officer …….
(GOVERNMENT M.O)

From Headmaster,
Kibaha Secondary School,
Date: ……

Name of Student …….....Date …… Term …..…… Year …….. I shall be very grateful if you will kindly examine the above named student and give us a report regarding his fitness to undertake studies well in our school.

A: PRELIMINARY INFORMATION: MEDICAL HISTORY

NO	DISEASE	YES	NO		DISEASE	YES	NO		DISEASE	YES	NO	
1.	Tuberculosis			7	Kidney/ trouble			13	Operation			19
2.	Asthma			8	Diabetes			14	Eye disorder			20
3	Pneumonia			9	Neverous breakdown			15	V.D			21
4	Heart trouble			10	Ear/Noise/Throat trouble			16	Disabled			22
5	Recurrent indigestion			11	Skin disorder/ disease			17				
6	Jaundice			12	Anaemia			18				

B: VITAL STATISTICS

Age …….. Height ……Weight …….. Blood group ……
Blood pressure ……. Pulse rate ……..
Systolic ……Diastolic …….

C: MEDICAL EXAMINATION:

	REMARKS/TREATMENT
EAR	RT. LT…….
VISION	RT. EYE LT. EYE
THROAT	
CHEST EXAMINATION	
ABDOMINAL EXAM.	LIVER SPLEEN
	OTHER COMMENTS
M.S. SYSTEM	UPPER LIMBS
	LOWER LIMBS
	SKIN
ANY OTHER FINDING	

D: LABORATORY EXAMINATIONS/INVESTIGATION:

(1) STOOL: - Ova ……..Leucocytes …….

(2) URINALYSIS: PROTEIN …….

GLUCOSE ……

SEDMENT: - OVA ……Leucocytes ……

(3) Hb ……

(4) B/S ……

(5) VDRL ……..

(6) WBC Total …….

Differential: N …….. L …… M …… E …… B ……

(7) X-ray Chest (If necessary) …….

(8) ANY OTHER INVESTIGATION……

MEDICAL CERTIFICATE:

We request the medical officer to complete the following:

I have examined the above named student and considered that he is physically fit/unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.

Date: ……Station ……Dr's Name: ……Signature ……

…….
GEORGE M. KAZI,
Headmaster,
KIBAHA SECONDARY SCHOOL.

SARE ZA SHULE

VAZI MBADALA LA DARASANI

VAZI RASMI LA DARASANI

VAZI LA KUSHINDIA

VAZI LA KAZI (SHAMBA DRESS)



VAZI MBADALA LA DARASANI